

**HOTUBA YA MGENI RASMI, KATIBU MTENDAJI WA  
NACTE KATIKA UZINDUZI WA TOVUTI NA NEMBO YA  
CHUO CHA HALI YA HEWA KIGOMA TAREHE**

**15 NOVEMBA 2018**

**Ndugu, Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa  
Tanzania;**

**Mkuu wa Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma;**

**Mameneja wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania;**

**Wakufunzi, Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma;**

**Wafanyakazi wa Chuo Cha Hali ya Hewa, Kigoma;**

**Wageni Waalikwa;**

**Wanahabari;**

**Mabibi na Mabwana,**

Awali ya yote kwa niaba ya Katibu Mtendaji, Baraza la Elimu ya Ufundi niliyemwakilisha napenda kumshukuru Mkurugenzi Mkuu pamoja na uongozi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kwa kuipa NACTE nafasi ya kuwa mgeni rasmi katika uzinduzi huu wa Tovuti na Nembo ya chuo.

**Ndugu Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Mkuu wa Chuo na Watumishi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania;**

Nimetiwa moyo na historia ya chuo uliyoitoa na naipongeza Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kwa kuanzisha chuo hiki ambacho ni chuo pekee nchini kinachotoa taaluma ya hali ya hewa katika ngazi ya cheti (NTA-Level 5) na diploma (NTA-level 6). Mafunzo haya ya hali ya hewa katika ngazi hii ya cheti na astashahada (Diploma) ni ya muhimu sana ukizingatia kwamba hii ndiyo kada tendaji katika ulimwengu wa kazi. Nchi yetu inakwenda kwenye uchumi wa kati au kuwa nchi ya Viwanda hivyo tunahitaji sana wataalamu wenye taaluma ya ngazi hizi. Wataalamu hawa ni muhimu kwa wananchi hasa wanaojishughulisha na kilimo. Pia nawapongeza kwa kuzingatia na

kufuata taratibu za uendeshaji mafunzo uliowekwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ili kutoa elimu bora yenye kukidhi viwango. Katika kumbukumbu za NACTE kuhusu chuo hiki kimesajiliwa kwa usajili wa kudumu 2014 na kwa sasa kipo katika mchakato wa ithibati (Accreditation). Aidha, chuo kimeendelea kuboresha huduma zake na hali hii inadhihirishwa na tukio la leo la uzinduzi wa tovuti yake. Kuwa na tovuti ya chuo pia ni moja ya vitu ambavyo NACTE inahimiza. Tovuti ya chuo ni muhimu sana na ina faida kubwa kwani hukitangaza chuo kwa upana sana kitaifa na Kimataifa.

Aidha, katika taarifa yako umesema kuwa kuna vyuo viwili tuu vya hali ya hewa katika ukanda wa Afarika Mashariki. Kwa hiyo, kwa tovuti hii chuo kitajulikana zaidi au kitawafikia watu wengi zaidi ndani ya nchi na jirani na hivyo kuongezeka kwa udahili. La muhimu ni kuhakiksha vigezo vya utoaji elimu vinafuatwa.

**Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania;**

Naipongeza Mamlaka kwa kubuni, kuweka kwenye mipango ya Mamlaka na kuweza kutengeneza tovuti hii itakayozinduliwa muda mfupi ujao. Tovuti hii itakidhi matakwa ya watumiaji wengi hasa wale wenye kutaka kupata taarifa za mafunzo yanayotolewa na chuo hiki na namna ya kuomba udahili. Kwa vile tovuti hii imeunganishwa na tovuti-mama ambayo ni ya Mamlaka ha Hali ya Hewa Tanzania itasaidia pia watumiaji kupata taarifa za hali ya hewa nchini ambazo ni za muhimu sana kwa wananchi, kwani sekta zote za maendeleo ya nchi tukianza na wananchi kwa ujumla wake, Kilimo, Afya, Nishati, Usafiri (wa anga, kwenye maji na nchi kavu), Elimu – mafunzo na tafiti mbalimbali, mazingira na zingine nyingi zinategemea taarifa zitolewazo na Mamlaka yenu.

**Mkuu wa Chuo cha Hali ya Hewa,**

Tovuti hii inao umuhimu mkubwa sana kwani itakuwa imewarahisishia kazi kwa kiasi kikubwa hasa kwenye kujitangaza

kwa ujumla. Kama Kaimu Mkurugenzi Mkuu alivyosema taaluma ya hali ya hewa inahitajika sana kwa maendeleo-endelevu ya nchi na nje ya mipaka ya nchi hivyo hakuna budi wananchi wakakifahamu chuo vizuri, aina ya mafunzo yatolewayo na gharama zake, muda wa mafunzo hayo na namna ya kutuma maombi ya kupata udahili. Kadhalika tovuti itakuwa imetatua changamoto ya kujitangaza nje ya mipaka ya Tanzania ambapo hapafikiki kwa urahisi kutumia vipeperushi ama magazeti. Tovuti ni njia sahihi kabisa.

**Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Mkuu wa Chuo na watumishi wa Chuo;**

Kwa upande wa NACTE tovuti hii itatupa fursa zaidi ya kushirikiana na chuo hasa kuhusiana na mambo ya udahili, mitihani na kadhalika.

Niwapongeze Mkuu wa chuo pamoja na uongozi kwa mawasiliano yenu ya mara kwa mara kuhusu masuala yanayohusu chuo kwani mara nyingi NACTE kama siyo moja kwa moja Makao Makuu Dar es Salaam, basi ni kwa kupitia ofisi zetu za Kanda zilizopo Tabora tumekuwa tukipokea simu zinazohitaji ufafanuzi mbalimbali kuhusu chuo. Niwapongeze sana kwani nasi tunapata

kujifunza zaidi namna ya kuboresha huduma zetu. Ni kwa namna hii mafanikio ya chuo yataendendelea kupatikana. Niseme tu kwamba, kupitia tovuti hii iliyo zinduliwa leo hii, NACTE pia tutaweza kwa namna moja ama nyingine kufaidika kwani tovuti na tovuti huwa zinaongea hivyo tutakuawa na ‘link’ kwenye tovuti zetu na kwa yale masuala yote yanayoshabihiana, kama ilivyo kwa tovuti hii ya chuo na tovuti-mama ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kwa jinsi alivyogusia Kaimu Mkurugenzi Mkuu.

**Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Mkuu wa Chuo, watumishi wa Chuo na Wageni waalikwa;**

Nachukua nafasi hii kuvipongeza vyuo vyote vilivyowakilishwa hapa ambavyo tayari vimekwishafikia hatua hii ya kuwa na tovuti yake. Aidha, natoa wito kwa wale wote ambao bado hawajapata tovuti wafanye hivyo mapema ili kurahisisha huduma na kuongeza ufanishi pamoja na uwazi katika utendaji.

Nawatakia wote mafanikio katika juhudi zenu za kuimarisha taaluma mbalimbali nchini na nje ya nchi.

**Asanteni kwa kunisikiliza na sasa niko tayari kuwazindulia tovuti na Nembo ya Chuo cha Hali ya Hewa Tanzania.**